

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA POLISI TANZANIA**



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA**

Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania anatangaza nafasi za ajira kwa vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), waliopo kwenye makambi na nje ya makambi wenye elimu ya kidato cha Nne, Astashahada, Stashahada, Stashahada ya juu na Shahada.

**1. Sifa za Waombaji**

- a) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.
- b) Awe amehitimu mafunzo ya JKT/JKU
- c) Awe amehitimu kidato cha nne kuanzia mwaka 2016 na kuendelea mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 25.
- d) Wahitimu wa Shahada, Stashahada ya juu na Stashahada wawe na umri kuanzia miaka 18 hadi 30.
- e) Awe na kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho kutoka mamlaka ya vitambulisho vya taifa (NIDA).
- f) Awe na afya njema kimwili na kiakili iliyothibitishwa na daktari wa serikali.
- g) Asiwe na kumbukumbu za uhalifu.
- h) Awe hajaoa/kuolewa au kuwa na mtoto.
- i) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (tattoo)
- j) Awe na urefu usiopunguwa futi tano(5.5) kwa wanaume, na futi tano inchi tatu (5'3") kwa wanawake.
- k) Awe hajawahi kutumia madawa ya kulevya.
- l) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya taaluma ya Polisi.
- m) Awe hajaajiriwa na taasisi nyingine ya serikali.
- n) Awe tayari kufanya kazi za Polisi mahali popote Tanzania.
- o) Waombaji watakaofaulu usaili ndio watakaochaguliwa.
- p) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili endapo ataitwa
- q) Kwa mwenye elimu ya Astashahada, Stashahada, Stashahada ya juu na Shahada awe na fani zilizoainishwa kwenye (kiambatisho 'A').
- r) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27/12/2022.

## **2. Utaratibu wa kutuma Maombi**

- i. Waombaji wote waandike barua za maombi wao wenyewe kwa mkono (Handwriting) bila kusahau namba zao za simu kwa anuani:  
Mkuu wa Jeshi la Polisi,  
S.L.P 961,  
DODOMA.
- ii. Kwa waombaji wa kidato cha nne ambao wameshahitimu mafunzo ya JKT/JKU na bado wapo makambini barua zao waziwasilishe kwa wakuu wa kambi.
- iii. Kwa waombaji wa kidato cha nne ambao wamehitimu mafunzo ya JKT/JKU waliopo nje ya makambi (uraiani), barua zao za maombi waziwasilishe kwa Makamanda wa Polisi wa Mikoa.
- iv. Kwa waombaji wenye elimu ya Shahada, Stashahada ya juu, Stashahada na Astashahada zilizoainishwa kwenye (kiambatisho 'A') watatakiwa kujaza fomu (kiambatanisho 'B') ambayo inapatikana kwenye tovuti ya Polisi inayoonyesha taarifa zake binafsi. Utumaji wa fomu hiyo usiwe kwa njia ya kuskani (Scan) ila unatakiwa kupakua (download), na kujaza taarifa husika kisha kuituma pamoja na maombi. Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe [admin.phq@tpf.go.tz](mailto:admin.phq@tpf.go.tz) na sio kwa njia ya posta. Maombi yatakwawasilishwa kwa mkono au kwa njia ya Posta hayatapokelewa.

## **3. Waombaji wote waambatanishe na nakala zifuatazo:**

- a. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- b. Nakala ya kitambulisho cha Taifa cha NIDA au namba ya NIDA
- c. Nakala ya cheti cha kuhitimu mafunzo ya JKT/JKU kwa walio nje ya makambi.
- d. Nakala za vyeti vya taaluma (Academic Certificates).
- e. Nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo ya sekondari (Leaving Certificates).

Imetolewa na:

**Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania**

**Makao Makuu ya Jeshi la Polisi**

**S.L.P 961**

**DODOMA**

**05/12/2022**